

Mbinu za Uundaji wa Maneno katika Luga ya Kirundi

¹Havyarimana Enock and ²Kamaro Consolée

1University of Burundi, Burundi

enochelle1@gmail.com

2University of Dar es Salaam, Tanzania

kamaroconsolee73@gmail.com

Machi, 2024

Abstract: As it is for other languages, Kirundi language has continued to create and incorporate new words from other languages, especially French language. This study therefore aimed to examine the Kirundi words in order to determine the methods used to create those words. This research was conducted in Burundi at the Teachers College (Ecole Normale Supérieure) where 30 students from the department of social sciences and humanities were involved in the collection of data for this study. This study was guided by the Theory of Scientific Terms (NIK) developed by Kiingi (1989). In addition, questionnaire and observation were used as data collection instruments. The results of the study revealed that the Kirundi language has created and introduced new words using methods such as: derivation, translation, repetition, assimilation, creation, shortening, compounding, introduction of Bantu words, transfer, and methods of smallness, averageness and size. This study concludes by recommending further studies on the formation of new words in Kirundi with an emphasis on the adequacy of the vocabulary of this language in social activities in Burundi. Finally, the relevant government authority is encouraged to increase efforts in the standardization of this language so that what is taught in school is compatible with the official use of Kirundi language.

Keywords: Kiswahili language, Western languages, word formation, Kirundi language, language policy

Ikisiri

Kama ilivyo kwa lugha zingine, lugha ya Kirundi imeendelea kuingiza maneno mapya kutoka lugha zingine, haswa lugha ya Kifaransa. Hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza maneno ya Kirundi ili kubaini mbinu zilizotumika kuunda maneno hayo. Utafiti huu ulifanyika nchini Burundi katika chuo cha walimu ENS (Ecole Normale Supérieure) ambapo wanafunzi 30 kutoka idara ya sayansi za jamii na lugha walihusishwa katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Kazi hii ya utafiti iliongozwa na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) iliyoasisiwa na Kiingi (1989). Aidha, mbinu za utafiti zilijumuisha dodoso na uchunguzi. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa lugha ya Kirundi imeunda na kuingiza maneno mapya kwa kutumia mbinu kama vile : utohoaji, tafsiri, uradidi, uambishaji, ubunifu, ufupishaji, uambatanishaji, uingizaji wa maneno ya kibantu, uhamishaji, na mbinu za udogo, wastani na ukubwa. Utafiti huu unahitimisha kwa kupendekeza taftiti nyangi zifanyike kuhusu uundaji wa maneno ya Kirundi kwa kutilia mkazo kwenye utosherezi wa msamiati wa lugha hii katika shughuli za kijamii nchini Burundi. Mwisho, mamlaka husika za serikali zinahimizwa kuongeza juhudu katika usanifishaji wa lugha hii ili kile kinachofundishwa darasani kiendane na matumizi rasmi ya lugha ya Kirundi.

Maneno ya msingi: lugha ya Kiswahili, lugha za kizungu, uundaji wa maneno, lugha ya Kirundi, sera ya lugha

1. Utangulizi

Zoezi la kuunda maneno linahusu ujenzi, uzalishaji au utengenezaji wa maneno mapya katika lugha fulani. Uundaji wa maneno mapya huchangia katika kukuza msamiati wa lugha ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Aidha, uingizaji wa istilahi mapya huchochewa na mabadiliko katika nyanja za uchumi, siasa, uhamiaji, utamaduni na maendeleo ya sayansi yanayotokea katika jamii ya lugha husika. Kevogo na Wenzake (2021) wanasema kwamba teknolojia ya kompyuta imepenyeza takribani kila kipengele cha maisha ya mwanadamu huku istilahi zikiwa kiungo cha kati katika mawasiliano ya kiufundi.

Uundaji wa istilahi ni muhimu sana, haswa katika lugha za kibantu, kama vile: Kiswahili, Kirundi, Kinyarwanda, Lingala, Luganda, Shona na kadhalika, sababu ikiwa ni ukosefu wa visawe ikilinganishwa na lugha za kizungu. Kwa mujibu wa Kiango (1995), ujenzi wa msamiati wa lugha ya Kiswahili unajumuisha asilimia kubwa sana ya maneno ya kukopwa kutoka Kiarabu, Kihindi, Kijerumani, Kiajemi, na Kiingereza. Were-Mwaro (2003), akiwanukuu Picht na Draskau (1985:32-33), anadai kuwa ‘matakwa ya kihistilahi katika nchi zinazoendelea hayapaswi kupuuzwa. Hapa...juhudi nyangi zinafanyika ili kuboresha vifaa vya mawasiliano vya kitaaluma kutokana na lugha asilia ambazo kwa sasa hazijaendelea kiistilahi’.

Lugha ya Kirundi ni mionganoni mwa lugha za kibantu ambazo zina uhaba mkubwa wa istilahi kutokana, mionganoni mwa sababu zingine, na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Sewangi (2007), akimnukuu Sager (1990 :22), anaeleza kwamba uundaji istilahi

unaweza kutokana na misukumo ya aina mbili: msukumo wa ugunduzi, na msukumo wa kuingiza maarifa mapya katika lugha kutoka lugha nyingine.

Kwa mujibu wa Matinde (2012:110), ‘uundaji wa maneno ni mabadiliko ya istilahi na muundo unaosababishwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika nyanja mbalimbali za jamii ili kukidhi dhima ya lugha kama chombo kinachojitosheleza katika mawasiliano’. Ili kukidhi haja hii, kuna mbinu mbalimbali faafu katika uundaji na ukuzaji wa istilahi zinazotumika katika lugha fulani. Lugha ya Kirundi imeathiriwa pakubwa kimsamiati haswa na lugha ya Kifaransa. Yapo maneno mengi yaliyoingizwa katika lugha ya Kirundi kutoka lugha zingine. Swali linalokuja ni kwamba, je, ni mbinu gani zinazotumika kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi? Je, mbinu za kuunda maneno mapya za lugha zingine za kibantu, kama vile Kiswahili, zinaweza kufaa kwa lugha ya Kirundi?

Kwa mantiki hii, makala hii inajadili mbinu za uundaji wa maneno katika lugha ya Kirundi kwa kutumia mifano kutoka lugha ya Kifaransa na Kiswahili. Aidha, mifano ya Kifaransa inafaa kwa kuwa lugha hii imeathiri kwa kiasi kikubwa msamiati wa lugha ya Kirundi. Vilevile, kutokana na uhusiano wa kiisimu uliopo kati ya lugha ya Kirundi na lugha ya Kiswahili, kazi yetu iliegemea kwa kiasi kikubwa katika tafiti husiani zilizofanywa katika lugha ya Kiswahili, kama lugha ya kibantu na ilioendelea sana kuliko lugha ya Kirundi. Kearns (2008) anadai kuwa lugha za kibantu ni lugha zenyenye uhusiano wa kumuundo na kimaumbo wa karibu sana.

2. Mapitio ya Maandiko

Katika sehemu hii, tunafafanua dhana ya neno, msamiati na istilahi. Vilevile, sehemu hii inachambua tafiti mbalimbali kuhusu mbinu za uundaji wa maneno mapya katika lugha ya Kiswahili, lugha ya kibantu kama ilivyo lugha ya Kirundi. Pia, sehemu hii inaeleza kuhusu haja ya kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi.

2.1 Dhana ya Neno, Msamiati na Istilahi

Neno ni kipashio kidogo zaidi kinachojihimili katika sentensi. Kiungo hiki, neno, huwakilisha maana inayokubalika katika sarufi ya lugha maalumu. BAKITA (2017) inafafanua kuwa neno ni tamko mojawapo mionganoni mwa mengi ambalo mtu hulitamka katika mchakato wa mazungumzo. Kwa mujibu wa Zabroni (2018), neno ni kipashio cha chini kabisa cha kisintaksia. Anaendelea kudai kwamba neno linawenza kuwa na maana ya kileksika au maana ya kisarufi. Kwa mfano, neno ‘kuimba’ lina maana ya kileksika na neno ‘ya’ lina maana ya kisarufi.

Kwa kawaida, neno ni sehemu fupi ya lugha yenyenye maana. Ni sauti inayotamkwa au kuandikwa pamoja na kutaja jambo fulani.

Kiuhalisia, uingizaji maneno mapya katika lugha fulani ni muhimu kwa sababu uundaji wa istilahi kwa ajili ya kuingiza maarifa mapya katika lugha hufanywa kwa kudhamiria na huzingatia kanuni mahususi. Pia, kwa mujibu wa ISO CD 704 (1997) misingi ya uundaji wa istilahi haina budi kuzingatia mambo matatu, ambayo ni mfumo wa dhana, ufanuzi wa dhana, na vitajo vya dhana au istilahi (Sewangi, 2007). Maneno ya lugha huwa yanagawanywa katika makundi mbalimbali. Zabroni (2018), akimmukuu Khamis (2009), anasema kuwa kila neno huweka katika kategoria au kundi lenye jina mahususi la kisarufi linalolitofautisha na maneno mengine kutokana, hasa, na kazi yake na umbo lake kimamatamshi na kiuandishi.

Upo uhusiano baina ya istilahi, msamiati na neno. Kwa mujibu wa BAKITA (2017), msamiati ni jumla ya maneno yote yaliyomo na yanayotumika katika lugha fulani. Msamiati ni jumla ya maneno yanayotumika katika lugha fulani. Hata hivyo, neno msamiati hutumika mara nyingi kumaanisha maneno mapya au maneno yasiyojulikana kwa watu wengi. Isitoshe, msamiati hutumika kufafanua maana ya maneno yanayopatikana katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano, tunapoongea juu ya msamiati wa hospitalini, tunarejelea maneno yanayotumika sana katika mazingira ya hospitalini, lakini hayatumiki kwa kiasi hicho kwingineko. Vilevile, istilahi ni maneno yanayotumika katika uga maalumu wa kitaaluma kama vile kompyuta, sayansi, tiba, au isimu.

Naye Nimessi (2022) anadai kuwa istilahi inaweza kufafanuliwa kwa namna nyingi tofauti. Kwanza, istilahi inaweza kufafanuliwa kama taaluma ya uundaji wa maneno. Pili, istilahi inaweza kujadiliwa kama jumla ya maneno yanayotumika katika uga maalumu. Mwisho, istilahi inaweza kuangaziwa kama kanzidata ya maneno yanayotumika katika fani maalumu.

kwa maelezo hayo yote kuhusu ‘neno’, ‘msamiati’ na ‘istilahi’, tunaweza kudai kwamba kuna uhusiano wa kidhana baina ya dhana hizo. ‘Neno’ hujumuisha msamiati na istilahi ilhali msamiati hujumuisha istilahi kwa kuzingatia taaluma ya uundaji wa maneno.

2.2 Haja ya Kuunda Maneno Mapya katika Lugha ya Kirundi

Ntiranyibagira na Bigirimana (2021) wanadai kuwa lugha asilia za Kiafrika zinadharauliwa sana dhidi ya lugha za kimataifa ambazo zimerithiwa kutokana na ukaloni, hivyo lugha ya Kirundi ni mionganoni mwa lugha hizo za Kiafrika.

Kirundi ni lugha rasmi ambayo inazungumzwa nchini kote Burundi (Sera ya Lugha ya Burundi, 2014:12), lakini lugha hiyo bado inakumbwa na changamoto kadhaa. Ntiranyibagira na Bigirimana wanaendelea kudai kwamba lugha ya Kirundi, katika uwanja wa

TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), inakumbwa na changamoto kubwa tatu zitokanazo na: kutafsiri kwenda Kirundi, kuunda maneno mapya, haswa kukopa na mwisho, changamoto zitokanazo na matumizi ya lugha kwa wazungumzaji wa Kirundi.

Ni bayana kwamba lugha ya Kirundi ina uhaba mkubwa wa istilahi. Na hilo huenda linachangiwa na ulumbilugha unaoshuhudiwa nchini Burundi, ambapo lugha nne zote zinatumika kwa ngazi ya kitaifa. Miongoni mwa lugha hizo nne zote ambazo zinafundishwa kuanzia elimu ya msingi mpaka elimu ya vyuo vikuu, tatu ni lugha rasmi- Kirundi, Kifaransa na Kiingereza (Sera ya Lugha ya Burundi, 2014:12).

Aidha, lugha ya Kirundi ina lahaja kadhaa ambazo zinapatikana katika mataifa jirani kama vile: Tanzania, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, maana yake ni kwamba lugha hii ina idadi kubwa ya wazungumzaji. Kiuhalisia, maendeleo ya sayansi na teknolojia, uhamiaji na miingiliano ya kijamii huifanya lugha kukua (Havyarimana, 2023), hivyo, zoezi la kuunda maneno mapya siyo jambo la kipekee kwa Kirundi bali ni uhai wa lugha zote duniani kama chombo muhimu cha mawasiliano. Kwa mujibu wa Sera ya Lugha ya Burundi (2014:4), uendelezaji wa lugha ya Kirundi ni jambo muhimu sana katika dunia inayoelekea kuwa kama kijiji kimoja, ambapo kunashuhudiwa maingiliano ya kitamaduni na kimatumizi ya lugha.

Kwa maana hiyo, uwepo wa maarifa juu ya mbinu za kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi utachangia pakubwa katika kukuza lugha hiyo. Vilevile, makala hii itakuwa muhimu sana kwa wafasiri na wakalimani ambao wanatatizwa sana na ukosefu wa visawe wakiwa wanahawilisha ujumbe kutoka haswa lugha za Ulaya, kama vile Kifaransa na Kiingereza kwenda lugha ya Kirundi (Ntiranyibagira na Bigirimana, 2021).

2.3 Mbinu za Uundaji wa Maneno katika Lugha ya Kiswahili

Wapo watafiti wengi waliojadili mbinu za kuingiza maneno mapya katika lugha ya Kiswahili. Kiango (1995) alianisha mbinu kadha wa kadha za kujenga istilahi mpya. Kiango (1995) alijadili mbinu ya ‘kubuni’. Yeye anadai kuwa njia hii inatumika katika hali kuu mbili. Kwanza, kuunda msamiati ambao utatumika kutaja vitu vinavyopatikana katika jamii ambavyo havijapewa msamiati wa Kiswahili. Pili, kuunda msamiati ambao utataja vitu kutoka nje ya jamii yenye msamiati wa kigeni. Anaendelea kudai kwamba kuna njia kuu mbili za kubuni msamiati. Kuna kubuni kinasibu; yaani, kuunda maneno kwa kuzingatia kanuni za kiisimu za lugha husika na kisha kuyapachika dhana mbalimbali, na kubuni kwa kuongozwa na vigezo maalumu, kama vile: maumbile, tabia, matumizi ya kitu kinachotakiwa kiundiwe msamiati wa Kiswahili.

Mtafiti huyu, alipendekeza ‘kukopa’ kama mbinu nyingine ya kuunda maneno mapya katika lugha ya Kiswahili. Yeye alijadili kwamba njia ya kukopa ni kongwe sana ikilinganishwa na mbinu zingine. Njia hii ni utaratibu wa kawaida unaojitokeza katika lugha nyingi duniani. Anaongeza kuwa mjengo wa msamiati wa lugha ya Kiswahili una asilimia kubwa sana ya maneno ya kukopwa kutoka Kiarabu, Kihindi, Kijerumanu, Kijemini, na Kiingereza. Kuna aina kuu mbili za kukopa. Kuna kukopa kwa kutohoa. Hii ni mbinu faafu kwa watumiaji wa lugha fulani ambapo mwanalugha anaitumia kwa kuhamisha msamiati wa lugha ya kigeni na kuuingiza katika lugha lengwa kwa kuzingatia fonolojia ya lugha husika. Nia ni kutumia neno lilelile lakini litamkike na liandikike kwa utaratibu wa Kiswahili. Mfano, office: ofisi, bacteria: bakteria. Kuna kukopa kwa kutafsiri. Njia hii inahu kutoa tafsiri za neno kwa neno za msamiati uliotumika kujenga dhana fulani.

Kwa mujibu wa Kiango (1995), kuingiza maneno ya kibantu na lahaja kunaweza kuwa mbinu ya kuunda maneno mapya katika Kiswahili. Mtafiti huyu anadai kuwa lajaja pamoja na lugha za kibantu zinaweza kusaidia kuziba pengo la msamiati katika lugha ya Kiswahili japo kwa kiwango fulani tu. Mbinu nyingine aliyoijadili ni mbinu ya kuhamisha maana. Hii ni njia ambayo neno fulani la Kiswahili hupewa maana mpya katika matumizi. Uchaguzi wa maneno haya utatakiwa kufanyika kwa umakini mkubwa; maana, siyo wa kiholela au kibahati nasibu; maneno yanayochaguliwa huibua fikra au dhana fulani.

Vilevile, kuna ‘kurakabu’ kama mbinu nyingine ya kuingiza maneno mapya katika lugha ya Kiswahili. Kiango (1995) anaeleza kwamba hii ni njia ambayo mtumiaji wa lugha husika anapanga maneno mawili au zaidi kwa lengo la kuunda neno jingine lenye maana ileile.

Pia, ufupishaji ulijadiliwa na mtafiti huyu kama njia ya kuunda maneno mapya katika lugha ya Kiswahili. Yeye anadai kuwa kuna vifupisho vya aina kuu mbili. Kuna vifupisho akronimu na vifupisho mchanganyo. Vifupisho akronimu hurejelea maneno yanayopatikana kwa kuunganisha sehemu ya kwanza au ya mwisho ya maneno mawili au zaidi ilhali vifupisho mchanganyiko huhusu maneno yanayopatikana kwa kuunganisha maneno mawili na kuwa neno moja. Kwa kawaida sehemu ya mwanzo ya neno la kwanza huungwa na sehemu ya mwisho ya neno la pili.

Kiango (1995) alibainisha pia ‘kunyambulisha’ kama mkabala wa kuunda maneno mapya katika Kiswahili. Mtafiti huyu anadai kuwa baada ya kuunda neno unaweza kupata maneno zaidi kwa kunyambulisha neno la kwanza. Kiango (1995) anadai kuwa njia hii ni njia ya kawaida katika lugha nyingi. Ni njia ambayo haina upinzani mkubwa.

Vilevile, ‘takriri’huweza kutumiwa katika uundaji maneno ya Kiswahili. Huu ni utaratibu ambao unachukua neno na kisha kulikariri. Matokeo yake ni kupata neno jipya lenye maana tofauti. Kadhalika njia hii haina upinzani mkubwa. Ni njia ambayo imeshamiri sana katika lugha ya Kiswahili.

Mtafiti mwingine aliyejadili mbinu za ujenzi wa istilahi katika lugha ya Kiswahili ni Maeda (2021). Yeye alijadili ‘unyumbuaji’ kama mkabala wa kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wake, njia hii inatumia mzizi mmoja wa neno na kujenga maneno mapya kwa kupachika viambishi nyambuaji. Mfano, soma ...somo kisomi msomi msomaji

Vilevile, mtafiti huyu alipendekeza ‘uambatishaji’ kama mbinu ya kuunda maneno mapya ya Kiswahili. Anadai kuwa hii ni njia ya kujenga istilahi mpya kwa kuambatanisha maneno mawili. Mfano, mwana+ diplomasia = mwanadiplomasia

Njia nyingine aliyoipendekeza ni ‘uradidi’. Maeda (2021) anahoji kwamba huu ni mchakato wa kurudiarudia neno au sehemu ya neno na kuunda neno jipya ambalo huwa na maana tofauti na maneno yanayorudiwarudiwa, mfano: tofauti= tofautitofauti, mbali= mbalimbali

‘Ufupishaji’ huweza kutumika kama mbinu ya kuunda maneno mapya. Mtafiti huyu anaeleza kwamba ufupishaji ni miongini mwa njia nyingine nyingi za kuundia maneno mapya. Anaonjeza kwamba ufupishaji unaojadiliwa hapa huweza kufanyika kwa njia mbili ambazo ni. Kufupisha kwa kuchukua herufi za mwanzo, mfano: CCM (Chama cha Mapinduzi), VVU (Virusi Vya Ukimwi) na kufupisha kwa kuchukua silabi za mwanzo za maneno yanayofupishwa, mfano: TAKUKIBU (Taasisi ya Kukuza Kiswahili Burundi), CHAKITABU (Chama cha Kiswahili cha Taifa Burundi).

Maeda (2021) alipendekeza njia nyingine ambayo ni ‘uhulutishaji’. Yeye anaeleza kuwa uhulutishaji ni mbinu ya kuingiza maneno mapya kwa kuchukua vijisehemu vya neno bila kuzingatia kanuni yoyote, mfano: chakula cha mchana - chamcha, hati za kukatazahataza

Vilevile, ‘utohoaji’ ulipendekezwa kama mbinu nyingine ya kuunda maneno mapya katika lugha ya Kiswahili. Mfatifi huyu anadai kuwa utohoaji ni uchukuaji wa maneno toka lugha moja na kuyatumia kwenye lugha nyingine baada ya kuyarekebisha kimamatishi na kimaandishi ili yaendane na sarufi ya lugha inayotoho, mfano: shirt= shati, radio= redio

Maeda (2021) alijadili ‘uchukuaji’ kama mbinu nyingine inayotumika kuingiza maneno mapya katika lugha fulani. Kwa mujibu wake, hii ni mbinu ya kuingiza maneno kwa kuyahamisha kutoka lugha yake asilia na kuyatumia kama yalivyo katika lugha nyingine. Uchukuaji hufanyika kwa lugha zinazoendana kisarufi kama Kiswahili na lugha ya Kirundi. Kubadili mpangilio wa fonimu. Mfano: lima – mila – imla – mali

Njia zingine alizozijadili ni kufananisha umbo/sauti /tabia, njia ya udondoshaji, mfano: mkwe wake – mkwewe, mwana wake – mwanawawe, ndugu yake – nduguye. Kuna pia mbinu ya kuzingatia matumizi ya kitu. Mfano: banio – (kubana), chanio – (kuchana), fyeko – (kufyeka), vilevile mbinu ya kutafsiri, mfano: Acquired immunal deficiency syndrome (Upungufu wa kinga mwilini), Human immunal virus – (virusi vya ukimwi)

Watafiti hawa hawatofautiani katika kueleza mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kuunda maneno mapya ya Kiswahili. Pia, tafiti hizi zinatoa mwanga kuhusu mbinu mbalimbali zinazotumika kuunda maneno mapya katika lugha mbalimbali, kwa kuwa hakuna lugha inayojitoshereza kimsamiati. Lugha ya Kiswahili imefanyiwa tafiti nyingi sana, tofauti na lugha ya Kirundi. Hivyo, kwa kurejelea tafiti mbalimbali katika uwanja wa isimu tumizi, kazi hii ililenga kuchunguza maneno mbalimbali ya Kirundi ili kubaini mbinu zinazotumiwa kuunda maneno hayo.

3.0 Nadharia ya Utafiti

Kazi hii ya utafiti iliogozwa na Nadharia ya Istilahi za Kisayansi (NIK) iliyoasisiwa na Kiingi (1989) na kuendelezwa na Kiingi (1992) na (1998); Were-Mwaro (2000) na (2001) pamoja na Kevogo (2020). Nadharia hii inafahamika kwa sifa saba maalumu zinazohusu lugha na uasiriaji upya wa istilahi. Sifa hizo ni pamoja na: Dhana za kimsingi, kipindi cha majaribio ya istilahi katika medani ya sayansi, kanuni ya uundaji dhana, kanuni ya geuza umbo kidhana, kanuni ya kidhana ya kuziba mapengo ya kiistilahi na vigezo vya istilahi zinazofaa vya PEGITOSCA. Vigezo vya istilahi zinazofaa vya PEGITOSCA vina dhima kuu katika uchunguzi unaofanywa katika kazi hii ya utafiti. Kiuhalisia, hivi ni vigezo vya kisayansi vya istilahi faavu vinavyotumika kuleta usasa na usanifu wa kimataifa katika shughuli ya ukuzaji wa istilahi. Vigezo tisa vinavyounda akronimu PEGITOSCA ambapo kwa Kiswahili vimefupishwa na kuitwa SIZAMASTALIHA ikiwa na maana ya usahihi, uiktisadi, uzalishi, umataifa, uangavu, ustaara, utaratibu, ulinganifu na uhalisia.

Hivyo, kwa kuongozwa na nadharia hii tuliweza kuchunguza maneno ya Kirundi na kubaini mbinu zinazotumiwa kuunda maneno hayo.

4.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza maneno ya Kirundi ili kubaini mbinu zilizotumika kuunda maneno hayo. Utafiti huu ulifanyika Burundi. Wango wa watafitiwa ulijumuisha wanafunzi 30 wa mwaka wa masomo wa tatu katika shahada ya awali, Idara ya Sayansi za Kijamii na Lugha ya Chuo cha Walimu (ENS). Watafitiwa waliombwa kutoa mifano ya maneno ambayo yanadhaniwa kuundwa kwa kutumia mbinu zilizokuwa zimeainishwa na mtafiti. Pia, mbinu ya uchunguzi ilitumika, ambapo maneno ya Kirundi alichunguzwa kwa kutumia maarifa ya mofolojia ili kubaini asili na muundo wake.

Aidha, mchakato wa uchanganuzi na uwasilishaji wa data za utafiti, ulifanyika kwa kuzingatia malengo ya utafiti ambayo ni kubaini mbinu za uundaji maneno katika lugha ya Kirundi. Aidha, mifano mingi inayohusisha matumizi ya lugha mbili imetolewa kwa Kifaransa na Kiswahili, na kutafsiriwa kwa Kirundi kwa kuwa lugha ya Kirundi imeathiriwa kwa kiasi kibwa na lugha hizo.

5.0 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inajadili mbinu tofautitofauti za kuingiza maneno mapya katika lugha ya Kirundi kulingana na matokeo ya uchanganuzi wa data zilizokusanya kwa wanafunzi wa mwaka wa masomo wa tatu katika shahada ya awali, Idara ya Sayansi za Kijamii na Lugha ya Chuo cha Walimu (ENS).

5.1 Utohoaji

Hii ni mbinu ambayo inatumika kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi. Mbinu ya utohozi au utohoaji wa maneno toka lugha moja na kuyaingiza katika lugha nyingine baada ya kuyafanyia marekebisho kimamatishi na kimaandishi ili yaweze kuendane na sarufi ya lugha lengwa.

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa lugha ya Kirundi imetoho maneno kadhaa kutoka lugha zingine, haswa lugha ya Kifaransa.

Hapa kuna mifano mbalimbali ya maneno yaliyoingizwa katika lugha ya Kirundi kutoka lugha ya Kifaransa kwa njia ya utohoaji.

Na.	Kifaransa	Kirundi
1	Avocat	Ivoka
2	Casier	Ikaziye
3	Fourchette	Ifurusheti
4	L'Etat	Leta
5	Moto	Imoto
6	Papaye	Ipapayi
7	Pile	Ipire
8	Quittance	Igitansi
9	Radio	Iradiyo
1.	Rideau	Irido

5.2 Tafsiri

Njia nyingine ya kuunda maneno mpaya katika lugha ya Kirundi ni tafsiri. Tafsiri ni njia ya kuingiza maneno katika lugha nyingine ambapo maneno husika au vifungu katika lugha chanzi hutafsiriwa katika lugha lengwa. Utafsiri wa aina hii huzingatia muundo wa lugha lengwa.

Ifuatayo ni mifano ya maneno yaliyoingizwa katika lugha ya Kirundi kwa njia ya tafsiri.

Na.	Kifaransa	Kirundi
1	Assiette	Isahani
2	Clou	Umusumari
3	Couteau	Imbugita/ Igisu/ Intambi
4	Cuillère	Ikiyiko
5	Maison	Inzu
6	Ordinateur	Inyabwonko
7	Pays	Igihugu
8	Province	Intara
9	Télévision	Imboneshakure
10	Vélo	Ikinga

5.3 Uradidi

Mbinu ya uradidi hutumika pia kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi. Mbinu hii inahusu kurudiarudia neno husika au sehemu ya neno na kutengeneza neno jingine ambalo huwa na maana tofauti na maneno yaliyokaririwa.

Kutokana na maelezo hayo, hii ni mifano ya maneno yaliyoundwa katika lugha ya Kirundi kwa njia ya uradidi.

Na.	Neno asilia (Kirundi)	Neno jipya (Kirundi)
1.	Cane	Canecane
2	Guhenda	Guhendahenda
3	Gusiga	Gusigasiga
4	Gusimba	Gusimbasiomba
5	Kugenda	Kugendagenda
6	Kuribwa	Kuribwaribwa
7	Kuvyimba	Kuvyimbavyimba
8	Munini	Muninimumunini
9	Muto	Mutomuto
10	Utujambo	Utujambojambo

5.4 Uambishaji

Hii ni njia ambayo inatumika sana katika uundaji wa maneno mapya. Mbinu hii inatumia mzizi mmoja wa neno na kuunda maneno mengine kwa kuongeza viambishi nyambuaji. Aidha, kwa kutumia mbinu hii neno hubadili kategoria yake. Kwa mfano, kitenzi huweza kugeuka jina.

Ifuatayo ni mifano ya maneno yaliyozalishwa kwa mbinu ya uambishaji:

Na.	Mzizi wa neno	Neno jipya
1.	Guhanura /ku-hanur-a/	Ubuhanuzi /u-bu-hanur-yi/
2.	Gukebura /ku-kebur-a/	Inkebuze /i-n-kebur-o/
3.	Gusigura /ku-sigur-a/	Umusiguzi /u-mu-sigur-yi/
1.	Gutamba /ku-tamb-a/	Intambo /i-n-tamb-o/
5.	Kubiba /ku-bib-a/	Umubivyi /u-mu-bib-yi/
6.	Kudandaza /ku-dandaz-a/	Umudandaza /u-mu-dandaz-a/
7.	Kugenda /Ku-gend-a/	Urugendo /u-ru-gend-o/
8.	Kurira /ku-rir-a/	Amarira /a-ma-rir-a/
9.	Kuririmba /ku-ririmba/	Indirimbo /i-n-ririmba/
10.	Kurongora /ku-rongor-a/	Umurongozi /u-mu-rongor-yi/

5.5 Ubunifu

Uundaji wa maneno mapya katika lugha ya Kirundi huweza kufanyika kwa kutumia mbinu ya ubunifu. Ubunifu ni njia ya kuunda msamiati mwingine katika lugha ya Kirundi na hurejelea dhana au vitu vipyta ambavyo hapo awali vilikuwa havipo katika jamii ya Warundi. Mbinu hii inapotumiwa, vipo vigezo mbalimbali ambavyo huwa vinazingatiwa kama vile: sauti ya kitu, sura au umbile la kitu, tabia ya kitu na matumizi ya kitu.

Vigezo hivyo vimejadiliwa kama ifuatavyo:

5.5.1 Sauti ya kitu

Hii ni njia inayotoa maneno yanayoashiria mlion au sauti ya kitu kinachohusika. Kama ilivyo kwa lugha ya Kiswahili, na lugha ya Kirundi imeingiza maneno mapya kwa njia ya ubunifu kwa kuzingatia sauti au mlion wa kitu husika.

Mifano:

Na.	Kifaa	Neno jipya
1.	Ikibati	Amanjanja
2.	Imoto	Ipikipiki
3.	Iradio	Isamirizi

5.5.2 Sura au umbo la kitu

Njia hii inahusu uundaji wa neno kwa kuzingatia sura au umbo la kifaa husika. Yapo maneno mbalimbali yaliyoingizwa katika lugha ya Kirundi kwa kufuata mbinu hii.

Ifuatayo ni mifano ya maneno yaliyoundwa katika lugha ya Kirundi kwa kuzingatia sura au umbo la kitu husika.

Na.	Kifaa/ Mtu	Neno jipyä
1.	Anayefanana na mbuzi	Gahene
2.	Anayefanana na mbwa	Ndura
3.	Chambre à air	Ishamburiyeri
4.	Msichana mrembo	Juru rya kurwa
5.	Mtoto wa kike mrembo	Akamarayika
6.	Mtu mnene	Umusozi
7.	Mtu mrefu	Umusumbaremba
8.	Mtu mweusi sana	Kaburimbo
9.	Mwanaume mzuri (Beau)	Rwagasore
10.	Pembe tatu	Inyabutatu

5.5.3 Tabia ya kitu

Maneno mapya huweza kuzaliwa kwa kuzingatia tabia ya kitu, haswa viumbe hai. Yapo maneno yaliyoingizwa katika lugha ya Kirundi kwa kuangalia tabia ya kitu, mnyama au ndege fulani.

Ifuatayo ni mifano ya maneno hayo :

Na.	Mtu	Neno Jipya
1	Anafanya kazi nyingi kwa wakati mfupi	Isirigit
2.	Anajifanya kama mtu mzuri	Inzoka
3.	Anakula sana	Isiha
4.	Anapenda kuimba	Umusani
5.	Anayegeuka watu	Ikivoruvo
6.	Anayekimbia sana	Umuravyo
7.	Anayekunyuwa pombe nyingi	Umuigina
8.	Anayetembea pole pole	Umusiba
9.	Mtu mwenye akili	Sungura
10.	Mwizi	Kaboko

5.5.4 Matumizi ya kitu

Katika lugha ya Kirundi, vifaa, majengo, na vifaa vingi vya kielekitroniki hupewa majina kwa kuzingatia matumizi yake.

Ifuatayo ni mifano ya maneno mapya yaliyoundwa katika lugha ya Kirundi kwa kuzingatia matumizi ya kifaa ama chombo husika.

Na.	Kazi	Neno jipyä
1.	Guca ibiti	Inryankwi/ incabiti
2.	Gufunyika	Umufuniko
3.	Gukerera	Urukero
4.	Gusamirana	Isamirizi
5.	Gusenya	Ishenyo
6.	Kuboha	Ibohero
7.	Kwerekana ibintu uri kure	Imboneshakure
8.	Kuvoma	Ikivomesho
9.	Kuvura	Ivuriro
10.	Kuyungurura	Akayunguruzo

5.6 Ufupishaji

Mbinu nyingine inayotumika kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi ni ufupishaji. Ufupishaji ni mbinu mionganini mwa mbinu zingine zinazotumika kuunda maneno mapya. Ufupishaji huweza kujitokeza kwa njia mbili.

5.6.1 Akronimu

Akronimu inahusu ufupishaji wa maneno kwa kutumia herufi au silabi za mwanzo wa neno.

Hii ni mifano kadhaa ya maneno yaliyoundwa katika lugha ya Kirundi kwa njia ya akronimu:

Na.	Kirefu cha maneno	Akronimu
1.	Itegereze Neza	I.N
2.	Menya Neza	M.N

5.6.2 Udondashaji

Huu ni ufupishaji ambao unahu sukuunda maneno mapya kwa kudondosha herufi ama silabi kadhaa za kiambajengo fulani.

Hii ni mifano ya maneno yaliyoundwa kwa kufuata mbinu ya ufupishaji kwa kudondosha herufi ama silabi kadhaa za vijenzi husika.

Na.	Vijenzi	Neno jipya
1.	Agakwavu	Gakwavu
2.	Akamaro	Kamaro
3.	Bujumbura	Buja
4.	Inangorore	Ngorore
5.	Inasenge	Senge
6.	Mbonyingingo	Mbonye
7.	Mukuru wiwe	Mukuruwe
8.	Murumuna wiwe	Murumunawe
9.	Mushiki wiwe	Mushikiwe
10.	Rwabuki	Buki

5.7 Uambatanishaji

Uambatanishaji ni njia maarufu ya kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi. Hii ni mbinu ya kuingiza maneno mengine katika lugha kwa kuunganisha maneno na kuyafanya kuwa neno moja lenye maana.

Yafuatayo ni baadhi ya maneno yaliyoundwa katika lugha ya Kirundi kwa kutumia mbinu ya uambatanishaji.

Na.	Vijenzi	Neno jipya
1.	Ikirira +habiri	Ikirirahabiri
2.	Imbonesha+ kure	Imboneshakure
3.	Inkono+ ya +itabi	Inkono y'itabi
4.	Inkuba + urujo	Inkubarujo
5.	Insimba + Urubebe	Insimbarubebe
6.	Soma+ kubika	Somambike
7.	Umunywa+ amazi	Umunywamazi
8.	Umushinga+ intahe	Umushingantahe
9.	Umushinga+amateka	Umushingamateka
10.	Umuvuga+ ubutumwa	Umuvugabutumwa

5.8 Uingizaji wa maneno ya kibantu

Lugha za kibantu kama vile: Kirundi, Kinyarwanda, Kiswahili, Lingala, na kadhalika, zina mwingiliano mkubwa kimsamiati. Ni rahisi kupata maneno ya Kirundi ambayo yanatumika katika lugha zingine za kibantu, haswa lugha za Ukanda wa Maziwa Makuu.

Ifuatayo ni mifano ya maneno yaliyochukuliwa kutoka lugha zingine za kibantu na kuingizwa katika lugha ya Kirundi

Na.	Lugha ya kibantu	Neno la Kirundi
1.	Amateka (Kinyarwanda)	Amateka
2.	Inteko (Kinyarwanda)	Inteko
3.	Karangwa (Kinyarwanda)	Karangwa
4.	Saa ngapi (Kiswahili)	Sangapi
5.	Saa sita (Kiswahili)	Sasita
6.	Sezirahiga (Kinyarwanda)	Sezirahiga
7.	Umutesi (Kinyarwanda)	Karibu
8.	Umutesi (Kinyarwanda)	Umutesi
9.	Urusimbi (Kinyarwanda)	Urusimbi
10.	Uwase (Kinyarwanda)	Uwase

5.9 Uhamishaji

Mbinu hii inatumika kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameifanya lugha ya Kirundi kuhamisha maneno kama yalivyo kutoka lugha za mataifa yaliyoendelea kisayansi na kiteknolojia. Mbali na hayo, lugha kama Kifaransa na Kiingereza zimepelekea ukiukwaji mkubwa wa kanuni za kiisimu za lugha ya Kirundi kwa kuchukua maneno kama yalivyo kutoka lugha hizo za kizungu. Ukiukwaji huo unajidhihirisha kwenye mofolojia na fonolojia ya maneno hayo.

Hii ni mifano ya maneno yaliyoingizwa katika lugha ya Kirundi kwa kutumia mbinu ya uhamishaji.

Na.	Lugha chanzi	Lugha lengwa
1.	Andika	Andika
2.	Kabisa	Kabisa
3.	Kaki	Kaki
4.	Karibu	Karibu
5.	Kwa	Kwa
6.	Mwa	Mwa
7.	Sawa	Sawa
8.	Shangazi	Shangazi
9.	Sungura	Sungura
10.	Wasiwasi	Wasiwasi

5.10 Udogo, Wastani, Ukubwa

Mbinu hii ni maarufu sana katika kuunda maneno mapya ya Kirundi. Pamoja na hayo, matokeo ya utafiti yilibainisha kuwa mbinu hii inatofautiana na mbinu ya unyambuaji wa maneno, kwa sababu maneno yanayozalishwa kwa mbinu hii huwa siku zote katika kategoría ya nomino kama ilivyo kwa maneno asilia.

Ifuatayo ni mifano kadhaa ya maneno yaliyotengenezwa kwa kutumia mbinu ya udogo, wastani na ukubwa

Na.	Udogo	Wastani	Ukubwa
1.	Agahugu	Igihugu	Uruhugu
2.	Agaka	Inka	Uruka
3.	Agasuka	Isuka	Urusuka
4.	Agatoke	Igitoke	Urutoke

5.	Agatore	Intore	Urutore
6.	Akagabo	Umugabo	Urugabo
7.	Akagore	Umugore	Urugore
8.	Akajumbu	Ikijumbu	Urujumbu
9.	Akana	Umwana	Urwana
10.	Akayiko	Ikiyiko	Uruyiko

6.0 Mchango wa Utafiti

Makala hii ilijadili mbinu mbalimbali za kuunda maneno katika lugha ya Kirundi. Umuhimu wa kazi hii ni kuchangia katika juhudu za kuendeleza lugha hii ambayo inakabiliwa na uhaba mkubwa wa msamati ikilinganishwa na hadhi na matumizi yake nchini Burundi. Vilevile, makala hii itachangia katika ufundishaji wa lugha ya Kirundi, haswa kwa ngazi ya shahada ambapo kozi za tafsiri hufundishwa. Umuhimu mwengine, makala hii itsaadia pakubwa wafasiri na wakalimani wa Kirundi katika kukabiliana na tatizo la usivisawe. Vilevile, kazi hii inaweza kuwa msingi wa tafiti zingine zinazolenga kukuza lugha hii ya Kirundi.

7.0 Hitimisho

Utengenezaji wa maneno mapya ni mabadiliko ya istilahi na muundo unaochangiwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika nyanja mbalimbali ili kuweza kukidhi mahitaji ya jamii husika. Utafiti huu ulijadili mbinu mbalimbali za kuunda maneno mapya katika lugha ya Kirundi. Mbinu zilizoainishwa ni kama: utohoaji, tafsiri, uradidi, uambishaji, ubunifu, ufupishaji, uambatanishaji, uingizaji wa maneno ya kibantu, uhamishaji, na mwisho mbinu ya udogo, wastani na ukubwa ilijadiliwa. Utafiti huu unahitimisha kwa kupendekeza tafiti nyingi zifanyike kuhusu uundaji wa maneno ya Kirundi kwa kutilia mkazo kwenye utosherezi wa msamati wa lugha hii katika shughuli za kijamii nchini Burundi. Mwisho, mamlaka husika za serikali zinahimizwa kuongeza juhudu katika usanifishaji wa lugha hii ili kile kinachofundishwa darasani kiendane na matumizi rasmi ya lugha ya Kirundi.

Marejeo

- BAKITA (2017 : Toleo la pili). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers (T) Ltd. Dar es Salaam.
- Havyarimana E. (2023). Unezi na Changamoto za Kiswahili Nchini Burundi. *Journal of Indigenous Languages*, Vol.1, No.1, 2023
- Kevogo, A. S. (2021). Ukopaji kama Mkakati wa Kuendeleza Istilahi za Tehama katika Kiswahili: Uchunguzi wa Vidahizo Teule vya Kamusi Sanifu ya Kompyuta. *CHALUFAKITA*, Juz. 3 Na. 1. (2021): 292-319.
- Kiango, J.G. (1995). Uundaji wa msamati mpya katika Kiswahili: zoezi lenye njia mbalimbali. *Kioo cha Lugha*, Juzu 1, Na.1
- Masebo, J. A. (2010). Nadhari ya Lugha Kiswahili 1. Dar-Es Salaam: Nyambari Nyangwine Publisher.
- Matinde, R. S. (2012). Dafina ya Lugha Isimu na Natharia. Kwa Sekondari, Vyuo Vya Kati na Vyuo Vikuu. *Mwanza: Serengeti Educational Publishers*.
- Mgulla, R.S. (1999). Mtalaa wa Isimu, Fonetiko, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili. *Nairobi Kenya: Longhorn Publishers*.
- Nimessi (2020). *La Terminologie*. Advanced School of Translators and Interpreters, University of Buea, Cameroon.
- Ntiranyibagira, C. (2019). Intra-Verbal Lexicalization of Transitive Forms in Kirundi. The Case of Reflexive and Applicative Affixes. *Palimpsest / Палimpseст*, 4(7), 47-54.
- Picht, H. na Draskau, J. (1985 :32-33). *Terminology: An Introduction*. University of Surrey, Department of Linguistics and International Studies
- Rubanza, Y. I. (1996). Mofolojia ya Kiswahili. Dar-Es Salaam : Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Were-Mwaro, A.G. (2003). Dhana ya Kubadilika kwa Lugha katika Isimu Historia-Linganishi : Mifano kutoka Kiswahili. Kiswahili. Vol. 66. P. 25-38
- Sera ya Lugha ya Burundi (2014).
- Sewangi, S.S. (2007). Uundaji wa Istilahi za Kiswahili Kileksikografia na Athari zake. *Nordic Journal of African Studies*. 16, 3 (Dec.2007).
- Zabroni, T. (2018). *Miundo Msingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Karljamer Publishers Limited: Dar es Salaam, Tanzania.